



DHIMA NA UJITOKEZAJI WA UKIMYA KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

Aldin K. Mutembei
Taasisi ya Taaluma za Kiswahili,
Chuo Kikuu cha dar es salaam
+255 222 410757 (Day time-Office)
+255 715 426 162 (Cell)
kaimutembei@gmail.com>

Baada ya elimu kuanza kupatikana vitabuni; na kwasababu ya kazi, wazazi wamehamishia sehemu kubwa ya malezi ya watoto wao mashuleni. Familia nyingi zimehamishia malezi ya watoto wao mashuleni. Huko kuna mkusanyiko wa staarabu mbalimbali kufuatana na mahali tofauti watoto watokako. Hata hivyo, kupitia katika vitabu na mitalaa, watoto wote huingizwa taratibu katika ustaarabu wa jamii moja inayofanana. Ni katika hali hii ambapo hatuna budi kuelewa yale yaliyomo katika vitabu hivyo, ili tufahamu jinsi malezi yatavyokuwa na kwamba wao watakuwa watu wa namna gani baadaye.

Mojawapo ya dhana inayojitokeza katika vitabu vingi vya fasihi ni ukimya. Ingawa ukimya huchipuka kutoka vyanzo mbalimbali (kama vile mtu binafsi, jamii na dini) na huletwa katika ufahamu wa watu kupitia katika jamii ukiwa na sura mbalimbali, hufanywa kuwa na sura moja inayokubalika au kuhimizwa kupitia katika vitabu vinavyosomwa mashuleni. Kwahiyo, kufahamu na kuchambua dhana hii ya ukimya ni jambo la msingi ili kuweza kujua namna ukimya wa aina mbalimbali unavyofanywa kuwa wa aina moja au wenye kushabihiana. Kwa upande mwingine, kumekuwapo na rai ya “kuvunja ukimya” katika harakati za kuukabili na kupambana na UKIMWI. Hatuwezi kuuvunja ukimya tusipoufahamu. Hatuwezi kuufahamu vema, kama hatuelewi sura za utokeaji wake na maana mbalimbali ambazo dhana hii hubeba.

Kwahiyo, tunakila sababu ya kuujua na kuuchambua ukimya. Makala hii itachambua jinsi dhana hii inavyojitokeza katika fasihi ya Kiswahili na maana yake katika malezi na makuzi ya watoto.